# SERA YA MISINGI NA KUJITOLEA KWA KIMSINGI
## IMANI NA KUJITOLEA KWA BODI YA SHULE YA PROVIDENCE

**Madhumuni**

Kuzingatia mageuzi ya kina na kukarabati kwa Shule za umma za Providence kwa ufanisi wa wanafunzi wote.

**Suala**

Providence, kama shule zote za jiji za wilaya, hukabiliwa na changamoto katika kuelimisha wanafunzi wetu wote kuendesha maisha ya ufanisi. Nyingi ya changamoto hizi zimepita udhibiti wetu na kuhitaji mabadiliko katika sera ya umma. Lakini hatutatumia kilichopita udhibiti wetu kama kisingizio cha kutofanya kila kitu ndani ya udhibiti wetu.

Shule za jiji zina nafasi za kipekee na jukumu kusaidia kila mwanafunzi – bila kujali taifa, pato, usaidizi wa familia, lugha ya kwanza, au heri ya elimu ya mbele – kutimiza Ndoto ya Marekani. Tunakumbatia nafasi hiyo na jukumu. Elimu ni haki. Tunachukua kwa umakini jukumu letu la kiadili kuona kwamba kila mwanafunzi hupokea elimu ambayo ni haki yao.

Shule za umma, isivyo biashara au shule zisizo za umma, hazichagui watakao hudumia. Tunahudumia wanafunzi wetu wote – tajiri na maskini, walio wengi na wasio wengi, wanafunzi ambao familia zao zimewatayarisha vyema kwa shule na wanafunzi ambao hawajawahi kwenda shule, wanafunzi ambao familia zao zilikuja nchini vizazi vya zamani na wanafunzi ambao wamewasili tu. Idadi yetu mseto inasukuma uwezo wetu kuhudumia wanafunzi wetu na familia zao kuliko mbeleni. Lakini tunathamini utofauti wetu kama mali: wanafunzi wetu hufaidi wakijifunza pamoja na kutoka kwa wenzao.

Shule zetu zinaweza na zinapaswa kufanya tofauti kubwa kwa wanafunzi wetu, lakini haziwezi kufanya hivyo pekee. Jamii yote – shule, wilaya, familia, washirika, biashara – ina jukumu la pamoja la ufanisi wa wanafunzi wetu. Shule zetu lazima zihudumu katika jamii yetu, na jamii yetu lazima ihimili shule zetu. Uhimili wa shule kwa jamiii na uhimili wa jamii kwa shule huongeza mtaji wa kijamii na mwishowe ufanisi wa wanafunzi wetu.

Kwa muda mrefu, shule zetu zimeangusha wanafunzi wetu wengi na kusukuma nje walio na njia na machaguo mengine. Utendaji umeboreka kwa miaka tano iliyopita, lakini wanafunzi wetu wanaendelea kutenda katika viwango vya chini sana kwa taifa, na utofauti kwa utaifa, hali ya kiuchumi-jamii, na lugha ya kwanza huendelea. Bodi ya Shule ya Providence inafanya bidii kubadilisha hilo. Shule za Providence lazima ziwe shule za chaguo la kwanza, sio mwisho, kwa familia zetu zote.

**Maadili ya Msingi**

Heshima, usawa, ufanisi, uwajibikaji, na uthamini kwa utofauti wetu

**Maono**

Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence itakuwa kiongozi wa taifa katika kuwafunza vijana wa jiji.

**Dhamira**

Shule za Providence zitawatayarisha wanafunzi wote kufaulu katika vyuo na vyuo vikuu vya taifa katika taaluma wanazozichagua.

**Imani na Kujitolea**

1. **Tunaamini wanafunzi wote wa Providence wanaweza na wanapaswa kujifunza katika viwango vya juu, kufikia uwezo wao kamili, na kufaulu shuleni na maishani**

Tunaamini—

- ✓ Uwezo wa kujifunza hauwekwi aidha wakati wa kuzaliwa wala kuamuliwa na rangi au kiuchumi-jamii; hukua kwa muda kwa fursa, msukumo, na juhudi.
- ✓ Ufanisi hujumuisha sio tu ufanisi wa kielimu tu, lakini pia kijamii, kihisia, kimwili, kisaikolojia, na ukuaji wa kimaadili.
- ✓ Ufanisi una maana kuchangia katika jamii na kushiriki katika maisha ya kiraia.
- ✓ Shule lazima zikuze upendo wa kusoma, kufunza watoto jinsi ya kujifunza, na kusaidia watoto kukuza talanta zao.
- ✓ Utofauti katika ufanisi wa elimu kwa misingi ya kirangi na kiuchumi haukubaliki kimaadili.
- ✓ Mafunzo ya mtaalamu, muda wa kutosha, na uhimili sahihi unaweza saidia kila mwanafunzi kufaulu.

**Tunajitolea kuunda mazingira kwa wanafunzi wote kujifunza katika viwango vya juu hadi uwezo wao kamili; tunajitolea kuziba mwanya wa ufanisi.**

Tuta**—**

- ✓ Sukuma kila mwanafunzi na kushikilia wanafunzi wote kwa matarajio sawa na dhahiri ya juu.
- ✓ Unda jamii changamfu, mahiri za mafunzo zilizo na nafasi zenye nguvu za elimu, za mtaala-sawa, na mtaala-ziada.
- ✓ Kupima ufanisi wa mwanafunzi kwa kile amejifunza, sio tu kile kimefunzwa.
- ✓ Tolea wanafunzi nafasi nyinyi na machaguo ya kufaulu**.**
- ✓ Unda jamii zilizo na imani na heshima za shule.
- ✓ Kuza afya na ustawi wa mwanafunzi.
- ✓ Unda mashirikiano ya mikakati na mashirika ya nje kustawisha huduma za uhimili wa mwanafunzi.

2. **Tunaamini walimu wa Providence na shule za Providence zinaweza na zinapaswa kuwa na ushawishi chanya na mvuto mkubwa kwa maisha ya wanafunzi wetu.**

Tunaamini—

- ✓ Mahusiano ya mwanafunzi-mwalimu ni kiini cha mafunzo.
- ✓ Mwalimu mshawishi huchukua jukumu kwa kile kinachotokea darasani na kuwajibika kwa kile kila mwanafunzi anajifunza.
- ✓ Hatimaye ni mwalimu ambaye anafanya tofauti katika ufanisi na kutofanikiwa kwa mwanafunzi.
- ✓ Shule ziko kuwasaidia mahusiano ya mwanafunzi-mwalimu; wilaya iko kusaidia shule.

**Tunajitolea kupanga shule zetu na rasilimali zetu kusaidia mahusiano ya mwanafunzi-mwalimu kama sababu kuu katika ufanisi wa mwanafunzi.**

Tuta—

- ✓ Kuwa na mwalimu wa ushawishi mkuu katika kila darasa.
- ✓ Kuwa na kiongozi imara wa mafunzo kama mkuu wa kila shule.
- ✓ Kuweka sera na kugawa rasilimali kwa kuuliza jinsi maamuzi yetu yanasaidia wanafunzi wetu kujifunza.

3. **Tunaamini shule za Providence zinaweza na zinapaswa kuwa mahali pazuri pa kufunza na mahali pazuri pa kujifunza.**

Tunaamini—

- ✓ Shule lazima ziwe na mazingira salama, ya kujali na yenye mpangilio yanayokuza kufunza na kujifunza kwa ufanisi.
- ✓ Shule lazima zithamini utofauti kati ya wanafunzi, wafanyikazi, na familia.
- ✓ Wanafunzi, wafanyikazi, na washirika wa jamii wanapaswa kuonyesha tabia ya

ukweli, maadili na isiyo baguzi.

**Tunajitolea kuunda shule zilizo na tamaduni chanya na kuwekwa katika vituo vya ubora wa juu.**

Tuta—

- ✓ Dumisha shule za kupendeza, safi, na salama
- ✓ Kukarabati au kubadilisha majengo ilivyo muhimu kujumuisha mafunzo ya karne ya 21 na kuhudumu kama nanga ya jamii.
- ✓ Shikilia wanafunzi, wafanyikazi, wazazi na washirika wa jamii kwa mienendo mahiri na viwango vya juu.

4. **Tunaamini wilaya ya shule ya Providence inaweza na inapaswa kuwa shirika la utendaji wa juu.**

Tunaamini—

- ✓ Watu na lengo huendesha utendaji wa juu.
- ✓ Lazima tushike roho na akili za watu wetu kwa maoni mahiri na shawishi kwa ufanisi wa wanafunzi pamoja na nafasi za kushiriki, kuungana, kufanya pamoja, na kufanya uamuzi kwa kushirikiana.
- ✓ Tunapaswa kuwa na uongozi wa maoni na usambaao na umakini usiokona kwa matokeo.
- ✓ Tunapaswa kutoa matokeo yanayopimika kwa malipo kwa ujitoleaji wa rasilimali za umma.

**Tunajitolea kupanga Idara la Shule la Providence ndani ya biashara yake kuu – kufunza na kujifunza.**

Tuta—

- ✓ Shikilia wilaya nzima na kila mtu ndani yake kujukumika kwa ufanisi wa mwanafunzi.
- ✓ Lenga rasilimali kwa vipaombele vya wilaya kwa kamili.
- ✓ Sajili, kuza, saidia, na kudumisha wafanyikazi walio na ubora wa juu.
- ✓ Kuendesha mifumo fanifu ya kufunza na biashara.
- ✓ Tumia rasilimali za umma kwa ufanisi.

5. **Tunaamini familia za Providence na jamii nzima ya Providence inaweza na inapaswa kuhimili ufanisi wa wanafunzi wetu.**

Tunaamini—

- ✓ Familia ndio waalimu wa kwanza wa wanafunzi wetu.
- ✓ Jamii yetu ina rasilimali tajiri za tamaduni kusaidia elimu ya wanafunzi wetu.
- ✓ Mfumo wa shule na jamii zinajukumika kwa wenyewe kwa ufanisi wa mwanafunzi.

**Tunajitolea kushirikiana na familia na jamii katika kuunda na kuhimili elimu ya wanafunzi wetu.**

Tuta

- ✓ Karibisha na kuhusisha familia na jamii zetu kama washirika wanaothaminiwa na watetezi wa elimu.
- ✓ Unda mawasiliano mazuri ya nyumbani-shule kwa kutoa njia rafiki kwa wazazi kuwasiliana nasi na kuwasiliana na familia katika lugha mahiri, na adilifu.
- ✓ Kutoa safu ya njia kwa familia kushiriki katika elimu ya watoto wao nyumbani na katika shule.
- ✓ Shiriki na jamii kuunganisha shule, wanafunzi, na familia na mali za jamii.

| | | |
|---|---|---|
| **Historia** | Imepitishwa: | Novemba 22, 2004 Azimio #11-22-04 |
| | Imerekebishwa: | 11, 2006 Azimio #12-16-06 |
| | Ilipitiwa: | Januari 24, 2008 |

Shule za Umma za Providence,
Rhode Island